

Public education Discover a world of opportunities

KUSOMA: KUJIFUNZIA NYUMBANI

HATUA ZA KUSOMA

Mtoto wako hupitia katika hatua mbalimbali wakati wanajifunza kusoma. Kumbuka kwamba watoto hujifunza kwa njia tofauti na katika viwango tofauti, kwa hivyo kuwa mvumilivu na kila wakati hamasisha juhudhi ya mtoto wako.

**Soma vitu kwa mtoto wako
anavyovifurahia ili waweze kujifunza
kupenda kusoma!**

Wasomaji wa kuigiza

Wakati mtoto wako anakua na kuendelea, wao huanza kuwa na moyo wakupenda vitabu na maneno wanayoyaona karibu nawao.

Wanaweza kuanza kukuiga wewe kwa kushika vitabu kwa njia sahihi, na kugeuza kurasa kwa makini na kujifanya kusoma kwa kutumia picha na kumbukumbu zao kwa kurudia hadithi. Wao pia husoma kutofautisha kati ya mbele na nyuma ya kitabu, huelewa kwamba maneno na picha ni tofauti, na kwamba maneno ya kuchapishwa yana ujumbe.

Unaweza kumsaidia mtoto wako kwa:

- Kusoma nao kila siku
- Kuhamasisha na kusifia jaribio lolote wakati anajaribu kusoma
- Kuwaonyesha kuwa picha inasaidia kueleza hadithi
- Kusoma habari zao wanazozipendela tena na tena - uzoefu hujenga kujiamini
- Si kuwakosoa wakati wakifanya makosa - kujifunza kusoma inachukua muda!

Kusoma kwa Majaribio

Katika hatua hii, mtoto wako mara nyingi husoma kwa kuangalia picha na kutumia kumbukumbu zao za hadithi. Pia hutambua baadhi ya maneno, lakini lengo lao ni juu ya maana ya maandishi badala ya kusoma kila neno vizuri.

Unaweza kumusaidia mtoto wako kwa:

- Kusoma nao kila siku
- Wahamasishe kujaribu kusoma na wasifu kwa kila jaribio wakati wanajaribu kusoma
- Zungumza na wao kuhusu sauti, maneno na makala ya kuvutia katika vitabu na maandiko mengine kama bandika, orodha ya ununuzi na magazeti
- Kuzungumza na wao kuhusu wahusika wa kitabu na historia
- Wahamasishe kutoa maoni juu ya kile kinachotokea katika hadithi
- Endelea kusoma hadithi wanazozipenda tena na tena.

**Zima televisheni. Ni rahisi kwa mtoto
wako kuwa makini wakati hakuna
usumbufu.**



Department of
Education

**Utakuta masomo zaidi kwenye
Vifurushi vya habari za nyumbani
kwenye education.wa.edu.au.**